

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: Na. 027-2660501

Fax: Na. 027-2660500

Barua pepe: Info@mkingadc.go.tz

Tovuti: www.mkingadc.go.tz



S.L.P. 6005,  
TANGA.

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. HW/MKG/D.35/27/179**

**11.03.2022**

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI 335 YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI YA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Kata, Vijiji na Vitongoji vya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.

### **A. SIFA ZA WAOMBAJI**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 mpaka 45
- ii. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- iii. Awe anamiliki simu janja Android (kuanzia 8.5 version) yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima. Aidha, simu janja hiyo Android isiwe aina ya Iphone.
- iv. Awe na barua pepe (email address) na nywila (password) inayofanya kazi
- v. Awe ni mkazi wa Kata husika na awe tayari kutekeleza majukumu ya zoezi husika katika Kijiji chochote kilichopo katika Kata hiyo.
- vi. Awe na uwezo wa kutambua na kusoma ramani za eneo analoishi

### **B. KAZI NA MAJUKUMU**

- a. Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- b. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- c. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi

- d. Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi
- e. Kazi hii itafanyika kwa muda wa takribani siku 10
- f. Malipo kwa siku itakuwa ni shilingi 15,000/=. Aidha, kutakuwa na shilingi 5,000/= kwa ajili ya nauli, mawasiliano na kifurushi cha internet kwa ajili ya kutuma taarifa).

### C. MAOMBI YAAMBATANISHWE

- 1. Nakala ya cheti cha kuzaliwa au nakala ya kitambulisho cha NIDA
- 2. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
- 3. Picha (passport size 2)
- 4. Barua ya maombi, ipitie kwa Mtendaji wa Kijiji husika anapoishi mwombaji

### D. JINSI YA KUTUMA

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu, barua pepe (email address). Maombi hayo yawasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kwa mkono au kupitia anwani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA**  
**S.L.P 6005**  
**TANGA**

Aidha, chini ya bahasha upande wa kulia iandikwe **AZM/MKG/D.35/232**

### E. TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe **16.03.2022** saa 09:30 alasiri

  
Zahara A. Msangi  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**MKINGA**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA**